HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO

MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 9 MACHI 2018 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI

1.0 WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

1.	Mhe. Rachel G. Nyangasi	-	Mwenyekiti wa Halmashauri/ Diwani Kata ya Chigela	- Mwenyekiti
2.	Mhe. Clemence A. Msulwa	-	M/Mwenyekiti wa Halmashauri/ Diwani Kata ya Iyogwe	- Mjumbe
3.	Mhe. Elizabeth G. Senyagwa	-	Diwani Viti Maalum	- Mjumbe
4.	Mhe. Maneno R. Kashinde	-	Diwani Kata ya Chakwale	- Mjumbe
5.	Mhe. Rajabu A. Mguhi	-	Diwani Kata ya Idibo	- Mjumbe
6.	Mhe. Mariana D. Mwigema	-	Diwani Viti Maalum	- Mjumbe
7.	Mhe. Stephano D. Mganga	-	Diwani Kata ya Msingisi	- Mjumbe
8.	Mhe. Danstan Mwegoha	-	Diwani Kata ya Gairo	- Mjumbe
9.	Mhe. Mathius T. Ligelele	-	Diwani Kata ya Mandege	- Mjumbe
10.	Mhe. Malima M. Maswaga	-	Diwani Kata ya Chanjale	- Mjumbe
11.	Mhe. Elizabeth M. Mlimba	-	Diwani Viti Maalum	- Mjumbe
12.	Mhe. Elias N. Cherehani	-	Diwani Kata ya Chagongwe	- Mjumbe
13.	Mhe. Wilson S. N. Mziwanda	-	Diwani Kata ya Nongwe	- Mjumbe
14.	Mhe. Omary A. Mwande	-	Diwani Kata ya Leshata	- Mjumbe
15.	Mhe. Saimon M.Mkamang'ono	-	Diwani Kata ya Mkalama	- Mjumbe
16.	Mhe. Yosia W. Muya	-	Diwani Kata ya Italagwe	- Mjumbe
17.	Mhe. Ibrahim M. Mbwana	-	Diwani Kata ya Magoweko	- Mjumbe
18.	Mhe. Hilda Mdaki	-	Diwani Viti Maalum	- Mjumbe
19.	Mhe. Rose M. Maloda	-	Diwani Viti Maalum	- Mjumbe
20.	Mhe. Mangapi W. Mdangu	-	Diwani Kata ya Kibedya	- Mjumbe
21.	Mhe. Frank M. Mbaigwa	-	Diwani Kata ya Ukwamani	- Mjumbe
22.	Mhe. Jeni J. Yohana	-	Diwani Viti Maalum	- Mjumbe
23.	Mhe. Pharles Ndoo	-	Diwani Kata ya Madege	- Mjumbe
24.	Mhe. John Digwagala	-	Diwani Kata ya Rubeho	- Mjumbe
25.	Ndg. Agnes M. Mkandya	-	Mkurugenzi Mtendaji (H/W)	- Katibu

2.0 WAJUMBE WASIOHUDHURIA

1.	Mhe. Ahmed M. Shabiby (Mb)	Mbunge Jimbo la Gairo	- Kwa taarifa

3.0 WATAALAM WALIOHUDHURIA:

1.	Ndg. Christopher Ndaga	-	Afisa idara ya Utumishi na Utawala
2.	Ndg. Andrea Mahinyila	-	Afisa Uchaguzi (W)
3.	Ndg. Abdi Ndila	-	Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
4.	Ndg. Magareth Cheche	-	Afisa Elimu Msingi (W)
5.	Ndg. Godfrey G. Lupembe	-	Kaimu Afisa Tehama (W)
6.	Ndg. Marry Mlaa	-	Mthibiti Ubora wa Elimu (W)
7.	Ndg. Hubert Minja	-	Kaimu Afisa Manunuzi (W)
8.	Ndg. Frank Kobelo	-	Kny:Mkaguzi wa Ndani (W)

9. Ndg. Heke Bulugu - Mhandisi wa Maji (W)
10. Ndg. Simon Masala - Meneja TARURA
11. Ndg. Olsola Sindila - Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (W)
12. Ndg. Elisia Mtesigwa - Meneja wa CHF (W)
13. Ndg. Gilbert Malegesi - Afisa Mtendaji Mamlaka ya Mji Mdogo Gairo
14. Ndg. Isaya Mihinzo - Afisa Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii (W)
15. Ndg. Victoria Komba - Kny: Kaimu Afisa Mipango, takwimu na ufuatiliaji
16. Ndg. Cuthbert Milaho - Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)
17. Ndg. Ebenance Kamomonga - Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W)
18. Ndg. Sarikieli Skoyo - Kny: Mganga Mkuu (W)
19. Ndg. Ambrose Majumba - Kaimu Mweka Hazina wa Halmashauri
20. Ndg. Gwakisa Mwambene - Mratibu wa TASAF (W)
21. Ndg. George Makacha - Mwanasheria wa Halmashauri
22. Ndg. Josephat Lyombo - Kny: Afisa Ujenzi
23. Ndg. Peter Kaswamila - Kny:Katibu tume ya Utumishi wa walimu (W)
24. Ndg. Irene Mawole - Kaimu Afisa Mtendaji Kata ya Kibedya
25. Ndg. Stella Ngomano - Kaimu Afisa Mtendaji Kata ya Chanjale
26. Ndg. Aneth Mpili - Afisa Mtendaji Kata ya Chakwale
27. Ndg. Sarah Nkwabi - Afisa Mtendaji Kata ya Msingisi
28. Ndg. Said Jumbe - Afisa Mtendaji Kata ya Idibo
29. Ndg. Alfred Sangala - Kaimu Afisa Mtendaji Kata ya Chigela
30. Ndg. Julius Mrema - Afisa Mtendaji Kata ya Ukwamani
31. Ndg. Yahya Kombo - Afisa Mtendaji Kata ya Madege
32. Ndg. Janeth Likonoka - Afisa Mtendaji Kata ya Leshata
33. Ndg. Given Willium - Afisa Mtendaji Kata ya Chigela
34. Ndg. Ishungisa Kazara - Afisa Mtendaji Kata ya Nongwe
35. Ndg. Amina Kulwa - Kaimu Afisa Mtendaji Kata ya Magoweko
36. Ndg. Felix Hinju - Kaimu Afisa Mtendaji Kata ya Chagongwe
37. Ndg. Sophia Nyamasagala - Kaimu Afisa Mtendaji Kata ya Rubeho
38. Ndg. Andrea Andrea - Kaimu Afisa Mtendaji Kata ya Mandege
39. Ndg. Tamson Mwafubale - Afisa Mtendaji Kata ya Mkalama
40. Ndg. Omary Tawakali - Afisa Mtendaji kata ya Italagwe

4.0 KAMATI YA ULINZI NA USALAMA (W):

1. Mhe. Siriel Mchembe - Mkuu wa Wilaya ya Gairo
2. SSP Ramadhan Kitanto - Mkuu wa Kituo cha Polisi Gairo
3. Ndg. Optatus Mkongwa - Mshauri wa Mgambo (W)
4. Ndg. Ditrum Mhoma - Afisa TAKUKURU
5. Ndg. Adam John - Katibu Tawala (W)

5.0 VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA:

1. Ndg. Shabani Sajilo - Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (W)
2. Ndg. Josephine Mbezi - Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (W)
3. Ndg. Issaya Semwenda - Mwenyekiti Chama cha wananchi CUF (W)
4. Ndg. Ebeneza Mwamengo - Mwenyekiti wa CHADEMA (W)

7.0 MWENYEKITI MAMLAKA YA MJI MDOGO GAIRO:

1. Mhe. Andrea M. Sendeha - Mwenyekiti Mamlaka ya Mji Mdogo

9.0 WAGENI WAALIKWA

1. Ndg. David Peter - Meneja CRDB
2. Ndg. Emily Dafa - Meneja NMB
3. Ndg. Peter Paula - Mratibu CCT
4. Ndg. Fikiri Maiba - Meneja TFS
5. Ndg. Agnitha Mpanda -

10.0 WAANDISHI WA HABARI:

1. Ndg. Praxeda Mtani - Mwandishi wa Habari TBC
2. Ndg. Godfrey Lusega - Mwandishi wa Habari Radio Abood FM
3. Ndg. Omaru Husein - Mwandishi wa Habari Star TV

11.0 SEKRETARIETI:

1. Ndg. Oswin Msanjala - Kaimu Katibu wa Mikutano
2. Ndg. Shakila Mrisho - Katibu Msaidizi wa Mikutano

MUHT. NA 01/24/2017. UTAMBULISHO NA MATANGAZO MBALIMBALI

(A) UTAMBULISHO

Kabla ya kufungua kikao Katibu aliwaomba wajumbe pamoja na wageni waalikwa kujitambulisha kwa majina na nyadhifa zao ili kufahamiana. Wajumbe walijitambulisha na kufahamiana.

(B) MATANGAZO MBALIMBALI

1. Taarifa ya kifo cha Mkuu wa Shule, Sekondari ya Chakwale

Mkurugenzi Mtendaji (H/W) alitoa taarifa ya kifo cha aliyekuwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Chakwale Marehemu Mwl. Valentine Mgani ambacho kilitokea tarehe 27 Februari 2018 katika Hospitali ya Mkoa Morogoro. Alifafanua kuwa Maiti ilisafirishwa na mazishi yalifanyika kijijini kwa Nundwe Mafinga Iringa.

2. Taarifa ya Kamanda wa TAKUKURU (W)

Kamanda wa TAKUKURU (W) Bw. Ditrum Mhoma, aliwaeleza wajumbe kuwa ni vema kila Mwananchi na viongozi wote wa umma wakajiepusha na masuala ya rushwa kwa kutopokea au kutoa rushwa kwa lengo la kufanikisha jambo lolote lile.

Alieleza kuwa hakuna aliye juu ya sheria hivyo kwa yeyote atakayejihusisha na vitendo vya rushwa, sheria itachukuwa mkondo wake.

Aidha, aliwashauri Wahe. Madiwani kuhakikisha wanasimamia ipasavyo miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa katika Kata zao.

3. Taarifa ya Mhandisi wa Maji (W)

Mhandisi wa Maji (W) aliwaeleza wajumbe kuwa, Mamlaka ya Mji Mdogo Gairo ilikumbwa na changamoto ya kukosekana kwa maji kwa muda wa siku tano, kuanzia tarehe 5 Machi 2018 hadi tarehe 8 Machi 2018 kutokana na changamoto ya kuharibika kwa miundombinu ya maji.

Alieleza kuwa ukarabati wa miundombinu hiyo umesuasua kutokana na kuchelewa kwa makabidhiano kati ya Halmashauri na Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Maji, Bw. Helmani Mundo ambaye aligoma kukabidhi ofisi kutokana na madai kwamba barua yake ya uhamisho ilikuwa imekosewa.

Alieleza kuwa ufuatiliaji ulifanyika ili kuhakikisha huduma ya maji inarejea kwa wananchi kwa wakati.

4. Taarifa kutoka kwa Meneja wa TARURA

Meneja wa TARURA (W) Mhandisi Saimon Masala Nkulu, aliwaeleza wajumbe kuwa katika Bajeti ya 2018/2019 TARURA imetenga jumla ya TShs Bilioni 10 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya barabara za mjini na vijijini katika Halmashauri ya Wilaya ya Gairo.

Alieleza kuwa, katika fedha zilizokuwa zimehamishiwa TARURA kutoka Halmashauri Tshs Bilioni 1.6 kiasi cha Bil 1 kilikuwa kimeshatumika na Tshs 600,000,000 ndio zilizokuwa zinaendelea kutumika katika kutekeleza shughuli mbalimbali.

Alifafanua kuwa jitihada kubwa zinafanyika ili kuhakikisha ifikapo mwaka 2020 barabara zote ziwe zinapitika

Aliwashukuru Wahe. Madiwani kwa kushirikiana na TARURA katika kupeana taarifa kuhusu barabara zote zinazotakiwa kufanyiwa marekebisho katika maeneo yao aliwaomba kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya matumizi bora ya barabara.

5. Taarifa kutoka kwa Meneja wa TFS

Meneja wa TFS Bw. Fikiri Maliba aliwaeleza wajumbe kuwa ni vema wakafuata sheria za uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu kama vile, mkaa, mbao au magogogo kwa kuwa na leseni,kibali au idhini.

Alisisitiza kwamba yeyote anayefanya kinyume atachukuliwa hatua za kisheria kwa kosa la uhujumu uchumi.

6. Taarifa ya Katibu Tawala (W)

Katibu Tawala (W) Bw. John Adam aliwaeleza wajumbe kuwa ni vema katika kutekeleza majukumu viongozi wakazingatia Sheria, kanuni na taratibu za kazi.

Alisisitiza Maafisa Watendaji wa Kata kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa haki hasa katika kutatua migogoro mbalimbali katika Kata zao. Aliagiza Vikao vya kisheria viitishwe kwa wakati.

7. Taarifa ya Kamanda wa Polisi (W)

Kamanda wa Polisi (W) aliwaeleza wajumbe kwamba, Jeshi la polisi pamoja na majukumu ya kusimamia masuala ya ulinzi na usalama. Jeshi hilo limekuwa linakabiliwa na changamoto ya Kesi nyingi za mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Alieleza kwamba wazazi wengi wamekuwa wakishindwa kufika mahakamani na hivyo kusabisha kesi nyingi za mimba kushindwa kupata hukumu. Alisisitiza wazazi kuwa makini katika kuwalea watoto wao.

8. Taarifa ya Wageni wa Village Schools Tanzania (VST)

Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ilipokea ugeni wa viongozi kutoka shirika la VST ambalo makao yao makuu yako Mkoani Iringa.

Alieleza kuwa lengo la ujio wa wageni hao ni kuweza kushirikiana na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo katika kuwekeza katika Elimu ya Sekondari hasa katika maeneo ya vijijini ambako watu wengi hawapati fursa ya kusoma sekondari pale inapotokea hawakuchaguliwa na Serikali. Alifafanua kuwa VST kwa kushirikiana na Kata husika hujenga shule katika moja ya kijiji walichopendekeza wananchi kwa ajili ya kutoa elimu kwa wanafunzi wasiuchaguliwa na Serikali kuendelea na masomo ya sekondari.

Alifafanua kuwa viongozi hao wameacha sera zao namna wanavyoweza kushirikiana na jamii katika kujenga na kuendesha shule zao, hivyo aliwataka wajumbe kusoma sera hizo na kuona namna wanavyoweza kuchangamkia fursa hiyo mapema katika kuboresha masuala ya huduma ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Gairo hasa kwa wale waliokosa fursa ya kuchaguliwa katika shule za Serikali.

MUHT. NA 02/3/2018. KUFUNGUA MKUTANO

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua Mkutano, akifungua mkutano huo Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe pamoja na kuelekeza mambo yafuatayo:

1. Alisisitiza jitihada zifanyike kwa kusajili wanachama wengi zaidi wa CHF aliagiza huduma ya afya kwa wananchi iboreshwe ikiwa ni pamoja na kuendelea kufungua zahanati mpya katika maeneo mbalimbali, alisisitiza kuhakikisha upatikanaji wa dawa katika zahanati hizo kwa kuwa Serikali inatoa fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa dawa.
2. Aliishukuru Serikali ya awamu ya tano kwa kutoa fedha ambazo zinasaidia Halmashauri kutekeleza na kusimamia uboreshaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja ujenzi wa miundombinu ya shule za Sekondari, Njungwa na Nongwe pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa, vyoo, Nyumba za walimu na madawati katika shule mbalimbali za Msingi na sekondari, ujenzi wa Ofisi mpya za Halmashauri, Ujenzi wa Kituo cha afya Gairo pamoja na zahanati,
3. Alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji (H/W) kwa kuhamasisha kilimo cha mazao ya Korosho na pamba aidha alimpongeza kwa kufanikisha upatikanaji wa mbegu hizo mapema.

4. Aliagiza ufuatiliaji uendelee katika kukamilisha mradi wa maji wa Serengeti ili kuboresha huduma ya maji kwa wananchi.
5. Alisisitiza ufuatiliaji ufanyike ili kuhakikisha wazazi wote wanaostahili kuwapeleka watoto wao shule, wanatekeleza.
6. Aliagiza ufuatiliaji ufanyike ili kuhakikisha ufunguzi wa Kituo cha Afya Chakwale unafanyika mapema.

Baada ya maelekezo hayo Mwenyekiti alifungua mkutano saa 5:10 asubuhi

MUHT. NA 03/3/2018. KUTHIBITISHA AGENDA

wajumbe walizithibitisha agenda zifuatazo kujadiliwa katika mkutano huo.

1. Utambulisho na matangazo mbalimbali i
2. Kufungua Mkutano.....ii
3. Kuthibitisha agenda.....iii - iv
4. Nasaha za Mkuu wa Wilaya ya Gairo v
5. Maswali ya Papo kwa Papo kwa Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi Mtendaji (H/W). vi
6. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari ya Mkutano ya Baraza la Madiwani wa tarehe 24/11/2017.....1 - 10
7. Taarifa ya yatokanayo na Mkutano ya Baraza la Madiwani uliyofanyika tarehe 24/11/2017 11-12
8. Kupitia na kujadili taarifa za kawaida kwa kamati za: 13-64
   i. Kamati ya uchumi, Ujenzi na Mazingira Robo ya Pili (Oktoba – Desemba 2017)
   ii. Kamati ya Elimu, Afya na Maji Kikao cha Oktoba – Desemba 2017
   iii. Kamati Shirikishi ya kudhibiti UKIMWI (W) Kikao cha Oktoba – Desemba 2017
   iv. Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango Kikao cha Oktoba – Desemba 2017
9. Taarifa ya Mkutano wa Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo.....65
10. Masuala ya kiutumishi.....66
11. Kufunga Mkutano 67

MUHT. NA 04/3/2018. NASAHA ZA MKUU WA WILAYA YA GAIRO

Kabla ya kumkaribisha Mhe. Mkuu wa Wilaya kutoa nasaha, Katibu alimkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa CCM (W) kuzungumza na wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti wa CCM (W) Bw. Shaban Sajilo aliwataka viongozi wote kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kazi.

Alimpongeza Mhe. Rais Dr. John Pombe Joseph Magufuli kwa kusimamia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015 ikiwa ni pamoja na kusimamia nidhamu kwa watumishi wa umma.

Alisisitiza wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa wachukuliwe hatua za kisheria. Aidha aliagiza ufuatiliaji ufanyike ili kuwachukulia hatua wote waliosababisha wananchi wa Mamlaka ya mji Mdogo Gairo kukosa huduma ya maji kwa takribani siku 5 bila sababu za msingi.

Mhe. Mkuu wa Wilaya Gairo aliipongeza Serikali kwa kuleta fadha kwa wakati kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aliwapongeza pia wataalamu kwa kusimamia vema matumizi ya fedha zinazoletwa na Serikali katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri.

Aliwaeleza wajumbe kuwa ufuatiliaji unaendelea ili kukamilisha mapema mradi wa maji wa Serengeti kwa lengo la kuboresha huduma ya maji kwa wananchi.

Alisisitiza wataalamu kufanya kazi kwa kufuata misingi ya sheria, kanuni na taratibu za kazi, alionya tabia ya baadhi ya watumishi kuwabambikizia kesi wananchi. Aliwasihi Polisi, Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji kutekeleza majukumu yao kwa kutenda haki.

Alisema, kamati ya ulinzi na usalama (W) imejipanga kuhakikisha inafanya ufuatiliaji wa masuala mbalimbali katika shule za msingi na sekondari ikiwa ni pamoja na masuala ya ufaulu usioridhisha, tatizo la kutojua KKK na mimba kwa wanafunzi.

Akizungumzia kuhusu utunzaji wa mazingira, alishauri ni vema TFS wakafanya ufuatiliaji ili kuona namna ya kupunguza bei ya gesi kwa lengo la kuwahamasisha wananchi kutumia Gesi kwa kupikia badala ya mkaa ambao ndio tegemeo la wananchi wengi kwa sasa na kupeleke auharibifu wa mazingira kwa kiasi kikubwa.

Aliwataarifu wajumbe kuhusu upatikanaji wa Kompyuta 25 ambazo ziligawanywa katika baadhi ya shule za msingi, Benki ya NMB Gairo ilitoa msaada wa madawati 100 ambapo halotel nao waliahidi kutoa muda wowote. Aidha ufuatiliaji unaendelea ili kupata kompyuta za kutosha kwa shule zote za msingi na sekondari.

Akihitimisha nasaha hizo alisisitiza ufanyike utaratibu wa kuhakikisha zahanati zote zinaboreshwa kwa kuwa na matabibu wa kutosha pamoja na kuwekwa huduma ya umeme.

MUHT. NA 05/3/2018. MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MWENYEKITI WA HALMASHAURI NA MKURUGENZI MTENDAJI (W)

Hapakuwa na maswali ya papo kwa papo kwa kuwa hakukuwa na mjumbe yeyote aliyewasilisha maswali kwa Mhe. Mwenyekiti kwa ajili ya ufafanuzi.

MUHT. NA 06/3/2018. KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 24 NOVEMBA 2017 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO YA HALMASHAURI.

Muhtasari ulisomwa, kuthibitishwa na kusainiwa na Katibu na Mwenyekiti ili kuwa kumbukumbu sahihi za mkutano huo.

MUHT. NA 07/3/2017. TAARIFA YA YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 24 NOVEMBA 2017 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO YA HALMASHAURI.

Taarifa ilisomwa na wajumbe waliagiza:

Ziandaliwe fomu maalumu ambazo Maafisa watendaji wa Kata watazitumia kwa ajili ya kutoa taarifa za mapato kwa Wahe. Madiwani wa Kata husika, Fomu hizo zisainiwe na Afisa Mtendaji Kata pamoja na Mhe. Diwani wa kata husika.

MUHT. NA 8/3/2018. KUPITIA NA KUJADILI TAARIFA ZA KAWAIDA KWA KAMATI ZA:

Wenyeviti wa Kamati zifuatazo waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu ya kamati zao kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba 2017.

i. **Kamati shirikishi ya kudhibiti UKIMWI Wilaya kikao cha robo ya pili Oktoba – Desemba 2017**

ii. **Kamati ya Elimu, Afya na Maji kikao cha robo ya Pili Oktoba – Desemba 2017**

Mhe. Wilson Mziwanda Diwani Kata ya Nongwe alitaka kufahamu Mpango wa serikali katika kurekebisha ikama kwa walimu wa ukanda wa milimani ambako kuna upungufu mkubwa unaosababisha matokeo ya shule hizo kuwa mabaya.

Ilielezwa kuwa idara ya Elimu imepokea fedha za EP4R ambazo zitatumika kwa ajili ya kurekebisha ikama ya walimu kwa shule za ukanda wa milimani kadri ya itakavyowezekana kulingana na kiasi hicho cha fedha. Aidha ilielezwa kuwa zoezi hilo la kurekebisha ikama ni endelevu.

Azimio;

Urekebishaji wa ikama kwa shule za ukanda wa milimani uzingatie jinsi

iii. **Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kikao cha robo ya Pili Oktoba – Desemba 2017**

iv. **Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kikao cha robo ya Pili Oktoba – Desemba 2017**

Mhe. Maneno kashinde Diwani Kata ya Chakwale aliomba ufanyike utaratibu wa kukamilisha mapema ujenzi wa zahanati ya Chakwale.

Ilielezwa kuwa ufuatiliaji unaendelea ili kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo mapema aidha, Mhe. Diwani aombe fedha za makadilio ya gharama zinazoongezeka katika kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo.

Wajumbe walikubaliana

Kaimu Afisa Mtendaji Mamlaka ya Mji Mdogo Gairo aliwaeleza wajumbe kuwa, kufuatia pendekezo la Timu ya Menejimenti ya Halmashauri kuanzisha kituo cha mabasi cha muda katika eneo la Bw. Salehe Shabiby lililopo Unguuroad Kata ya Magoweko, wajumbe wa kikao cha Kamati ya Fedha katika Mamlaka ya Mji Mdogo Gairo waliipokea taarifa hiyo waliijadili na kuipitisha. Alieleza kuwa Mdau alitoa mashrti 3 kama ifuatavyo.

1. Mdau huyo akarabati eneo hilo kwa kujenga stendi na katika mgao yeye apate 60% na Halmashauri ipate 40%
2. Halmashauri ikarabati eneo hilo kwa kujenga stendi na katika mgao ipate 60% na mdau huyo apate 40%.
3. Mdau huyo alihitaji apewe mkataba wa miaka mitano (5)

Alifafanua kuwa mdau huyo iwapo ataaingia mkataba na Halmashauri atatekeleza yafuatayo;

1. Makusanyo yote ya mapato yatakusanywa kwa kutumia mashine (POS).
2. Atajenga banda kwa ajili ya kupumzikia wasafiri.
3. Atajenga choo cha matundu 8 (Me-4 na Ke -4)

Aidha katika majadiliano hayo Mamlaka ya Mji Mdogo ilishauri yafuatayo;

1. Mkataba uwe ni wa miaka 3 badala ya miaka 5 kama Halmashauri ilivyokubaliana na Bwana Salehe shabiby.

2. Afisa ujenzi afanye tathmini ya gharama zitakazotumika katika ujenzi wa kituo hicho ili kuwa na hesabu sahihi katika kipindi cha kuwekeana mkataba.
3. Walishauri kujengwa choo cha kudumu katika eneo hilo la kituo cha mabasi.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walitoa hoja zifuatazo;

1. Ili kuweza kufahamu namna ya kugawana faida kati ya Halmashauri na Mdau ni vema ikafahamika gharama atakazotumia mdau katika ujenzi wa kituo hicho cha mabasi.
2. Ni vema ikaundwa kamati itakayofuatilia utekelezaji wa ujenzi wa stendi hiyo kwa kujiridhisha kuhusu eneo la ujenzi na kufanya mazungumzo na mdau kuhusu namna ya kuingia mkaba naye.

Azimio;

Wajumbe waliagiza taratibu za ujenzi wa kituo cha mabasi cha muda ziendelee.
Kamati ndogo iliyowahusisha, Mhe. Danistan Mwegoha, Mhe. Elizabeth Senyagwa na Mhe. Andrea Sendeha pamoja na wataalamu ifanye mazungumzo na Bw. Salehe Shabiby ili kumwomba gawiwo la faida liwe 50% kwa 50% badala ya 40% kwa Halmashauri na 60 kwa Bw. Salehe Shabiby kama alivyohitaji aidha mazungumzo yafanyike ili mkataba uwe wa miaka 3 badala ya Mitano

MUHT. NA 09/3/2018. MASUALA YA KIUTUMISHI

Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa Baada ya Baraza kujigeuza Kamati na lilijadili masuala mawili ya kiutumishi na kuazimia yafuatayo:

9.1. Watumishi 10 waliosimamishwa kazi kwa maagizo ya Mhe. Waziri wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na utawala Bora kutokana na suala la kumlipa mshahara na kumhidhinishia mkopo Mwalimu Jasper Ibrahimu Luchelo wa Shuel ya sekondari Dumila ambaye hakuwepo kituo cha kazi tangu mwaka 2009.

Maazimio;

1. Kaimu Mweka Hazina Bw. Ambrose Majumba arudishwe kazini
2. Mweka Hazina Ndg. Ako Tu Ai arudishwe kazini
3. Mweka Hazina Ndg. Vikilile Mayenga arudishwe kazini
4. Afisa Utumisi na Utawala Ndg. Alice Lugata taratibu za kiutumishi ziendelee.
5. Afisa utumishi na Utawala Ndg. Juma Kongoi yeye alishastafu hivyo tuhuma hii ilikuwa akiwa ameshastaafu.
6. Kaimu Afisa utumishi na Utawala Ndg. Karorine Mbweni taratibu za kiutumishi ziendelee.
7. Kaimu afisa Utumishi na Utawala Ndg. Susan Nyanda taratibu za kiutumishi ziendelee.
8. Afisa Utumishi kitengo cha Lowson Ndg. Halima Sendoro taratibu za kiutumishi ziendelee.
9. Afisa Elimu Sekondari (W) Ndg. Godlove Nko taratibu za kiutumishi ziendelee.
10. Kaimu afisa Elimu Sekondari (W) Ndg. Elisadiki Ndosi taratibu za kiutumishi ziendelee.

9.2. Suala la Mtumishi Alex Gereza Afisa Kilimo anayekabiliwa na kesi ya kubaka
Ilielezwa kuwa Mtumishi huyu mahakama haikumkuta na hatia hata hivyo Baraza lilimsimamisha kazi na kuagiza taratibu za kiutumishi ziendelee.

10. MUHT. NA 09/24/2017. KUFUNGA MKUTANO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe pamoja na wageni waalikwa wote kwa kushiriki Mkutano huo. Aidha aliwaagiza wakuu wa idara kuhakikisha yote yaliyoazimiwa yanapatiwa majibu katika Mkutano wa Baraza la Madiwani ujao. Baada ya maelezo hayo aliwatakia safari njema na alifunga Mkutano saa 9:34 alasiri.
Naomba kuwasilisha.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA

..... **.....**
KATIBU **MWENYEKITI**

TAREHE.....